Oktoba 9, 2019

# Kijarida cha Mountain View

## Ujumbe wa Mwalimu Mkuu

Mwaka huu tunaangazia kuwa na itikadi ya shule iliyo salama na inayoakaribisha. Mojawapo kati ya malengo yetu ni kuamkua kila mtu kwa tabasamu, na kufanya tuwezayo ili kumfanya kila mtu ahisi utulivu na ahisi kuwa amekaribishwa. Walimu pia wanawaamkua wanafunzi wao wote kwa majina kila asubuhi. Haya yataifanya Mountain View iwe na mazingira mazuri. Hivi karibuni nilisoma kazi ya nyumbani ya kuandika iliyofanywa na mwanafunzi. Aliandika, "Ninapenda watu wanaponiambia habari. Inanifurahisha sana. Ninapenda jinsi walimu na wanafunzi wanavyofanya nihisi kuwa hapa ni pahali salama pa kupokea mafunzo." Wanafunzi wote wanafaa kuhisi hivi kuhusu shule, na tunafanya juhudi ili kuhakikisha kuwa hayo yanafanyika. Pia, kila mtu anaweza kusaidia. Ni jukumu la kila mtu kuwa mcheshi, mpole, na mwenye kukaribisha vizuri. Hivi karibu nilisikia habari kuhusu mwanafunzi aliyewaalika wanafunzi wenzake waliojiunga na shule karibuni ili wacheze na yeye. Mwanafunzi huyo ni shujaa wa Mountain View, na ni mfano murwa wa jinsi wanafunzi wanaweza kuchangia ili kuimarisha itikadi ya shule yetu.

## Lango Lililozibwa la Sehemu ya Kuegesha Magari Kabla na Baada ya Shule

Kwa kuwa tunaendelea kutafuta njia salama kabisa za watoto kuwasili na kutoka shuleni, tumegundua kuwa tukiziba lango kuu la sehemu yetu ya kuegesha magari, msongamano unakuwa mchache zaidi na wanafunzi wetu wanaweza kupita kwa usalama zaidi. Ikiwa unawachukua au unawabwaga wanafunzi shuleni kwa kutumia gari, tafadhali tumia lango lililoko mbele ya shule na tumia upande wa kulia ili kubwaga wanafunzi na upande wa kushoto ili kupita. Tafaddhali epuka kuegesha gari kwenye sehemu nyekundu unapowaingiza watoto shuleni. Pia, kumbuka kuwa tuna sehemu ya kubwaga/kuchukua watoto kwenye upande wa magharibi wa shule ambayo inasaidia kupunguza msongamano kwenye sehemu kuu ya kuegesha magari. Ni njia mbadala iliyo murwa.

## Shughuli Inayopendekezwa ya Kuongeza Kiwango cha Kuzingatia Hisia za Wengine cha Mtoto Wako

Kuzingatia hisia za wengine ni uwezo wa kuelewa na kuhisi wasiwasi wa mtu mwingine. Ni uhodari muhimu wa kijamii/kihisia ambao sisi sote tunahitaji kuukuza. Dkt. Michele Borba anapendekeza kitu kimoja kinachoweza kufanywa nyumbani ili kusaidia ukuaji wa uwezo wa kuzingatia hisia za wengine kwa watoto wetu ni kuwaambia wawaze kuwa wana kasoro ambayo kwa sasa hawana. Changamoto yoyote ambayo haijawahi kumfika mtoto wako inaweza kuhusishwa hapa. Lengo ni kumsaidia aitazame hali kutoka kwenye mwonekano wa mtu mwingine ambaye ana changamoto tofauti na yeye. Kisha tunamwambia aandike, aongee, au achore mwonekano wako wa vile angehisi iwapo itabidi yeye mwenyewe apitie hali hiyo.



## Matukio ya ujao

**Ijumaa, Oktoba 11**
Wazazi na Vitafunio/Baraza la Jumuiya ya Shule, 8:30, CLC
**Alhamisi, Oktoba 17**
Hakuna Shule, Likizo ya Msimu wa Kupuputika kwa Majani
**Ijumaa, Oktoba 18**
Hakuna Shule, Mapumziko ya Majira ya Kupukutika kwa Majani
**Jumatatu, Oktoba 21**
Hakuna Shule, Mapumziko ya Majira ya Kupukutika kwa Majani
**Ijumaa, Oktoba 25**
Chanjo za Bure za Homa ya Mafua, 12:00-6:00, CLC

## Wazazi na Mifugo

Kila asubuhi ya Ijumaa wazazi wana nafasi ya kujifunza kuhusu mfumo wa elimu, kukutana na kitivo na wafanyakazi wa shule, na kujadili masuala muhimu katika uzoefu wa watoto wao shuleni. Tunakualika ufike siku ya Ijumaa na uwe sehemu ya majadiliano haya. Tunakutana saa 8:15 katika Kituo cha Masomo cha Jumuiya, Chumba 182. Ikiwa unahitaji msaada kukipata, wafanyakazi wetu katika ofisi watakusaidia kupata maelekezo ya njia sahihi. Natumai kukutana nawe!

## Baraza la Jumuiya ya Shule

Halmashauri ya Jumuiya ya Shule (SCC) itakutana Jumatano ya kwanza ya kila mwezi katika maktaba yetu ya shule. Mkutano wetu ujao utakuwa TBA. Mikutano ya SCC ni wazi kwa umma.

## Fuata au Uwe Rafiki wa Shule ya Mountain View kwenye Mitandao ya Kijamii

Facebook: @MountainViewSLC
Twitter: @mtviewlibrary
Tunatarajia kuwa utatufuata, na tunatumai kuwa utaalika jamaa na marafiki ili kutufuata, pia.

## Masomo katika Kituo cha Kujifunzia Jumuiya (CLC)

Kituo chetu cha Kujifunzia Jumuiya kinatoa masomo mengi kwa ajili ya wanafunzi na watu wazima. Tafadhali tembelea ofisi za Kituo cha Kujifunzia Jumuiya ili ujipatie kalenda husika. Mtu yeyote wa jumuiya yetu anakaribishwa kujiandikisha na masomo.

Hakuna mfanyakazi wa wilaya au mwanafunzi watakuwa wanakabiliwa na ubaguzi katika ajira au mpango wowote wa wilaya au shughuli kwa misingi ya umri, rangi, ulemavu, jinsia, utambulisho wa kijinsia, maelezo ya jeni, asili ya kitaifa, ujauzito, rangi, dini, ngono, au mkongwe hali. wilaya ina jukumu la kutoa fursa sawa na nafasi sawa katika mipango yake, huduma na ajira ikiwa ni pamoja na sera zake, taratibu malalamiko, mpango upatikanaji, matumizi kituo wilaya, makao na sawa ya ajira mambo mengine Nafasi. wilaya pia inatoa fursa sawa ya vifaa wilaya kwa ajili ya makundi yote ya vijana waliotajwa katika Title 36 ya Marekani Kanuni, ikiwa ni pamoja na makundi scouting. mtu ifuatayo imetafsiriwa mteule kushughulikia maswali na malalamiko kuhusu ubaguzi kinyume cha sheria, unyanyasaji, na kulipiza kisasi: Tina Hatch, Mwafaka na Uchunguzi, 440 East 100 South, Salt Lake City, Utah 84111, (801) 578-8388. Unaweza pia kuwasiliana na Ofisi ya Haki za Kiraia, Denver, CO, (303) 844-5695.